

**SALAMU ZA OFISI YA MAKAMU WA RAIS WAKATI MAZISHI YA MZEE  
HASANIELI ELISAEI MREMA, OLD MOSHI, MDAWI – MKOANI  
KILIMANJARO TAREHE 8 MEI, 2024**

**Ndugu Waombolezaji:**

Kwanza kabisa napenda niungane na waombolezaji wenzangu kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa Mzee wetu mpendwa sana, Hasanieli Elisaeli Mrema ambaye Mwenyezi Mungu amemwita kwake. Naomba kwa heshima niwasilishe kwenu salamu za pole kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Ndugu Waombolezaji:**

Mzee Hasanieli Elisaeli Mrema alikuwa ni mmoja wa vijana walioshiriki tukio la kuchanganya udongo wa Tanganyika na Zanzibar lililofanyika tarehe 26 Aprili, 1965 katika sherehe za mwaka mmoja wa Muungano zilizofanyika katika Uwanja wa Uhuru, Jijini Dar es Salaam. Alishiriki katika tukio hilo akiwa kijana mwenye umri wa miaka 20 pamoja na wenzake watatu (Mzee Hassan Omari Mzee kutoka Zanzibar, Bi. Khadija Abasi Rashid kutoka Zanzibar na Bi. Sifael Mushi kutoka Tanzania Bara hapa Kilimanjaro).

**MCHANGO WAKE KATIKA MUUNGANO**

**Ndugu Waombolezaji:**

Ofisi ya Makamu wa Rais inatambua na kuthamini mchango wake mkubwa katika kuudumisha Muungano wetu adhimu hususan ushiriki wake katika tukio adhimu la kuchanganya udongo wa Tanganyika na Zanzibar. Mzee Mrema hakusita wakati wote kueleza uzuri na faida za Muungano na kutoa wito kwa Watanzania hususan vijana kuulinda na kuutetea Muungano wetu. Wakati wote alipoombwa kuhojiwa n awaandishi wa habari, hakusita kufanya hivyo.

Tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa maisha yake na tutazikumbuka nyakati zote ambazo tuliweza kushiriki naye katika matukio muhimu ya Kitaifa hususan sherehe za Muungano ambapo yeye na wenzake watatu (Mzee Hassan, Bi. Sifael na Marehemu Bi. Khadija) walishiriki kwa pamoja katika sherehe za Muungano zilizofanyika Tanzania Bara (Dar es Salaam na Dodoma) na Zanzibar pia.

**Ndugu Waombolezaji:**

Ofisi ya Makamu wa Rais pia iliwahi kuwaalika wazee wetu Bungeni wakati wa kusoma hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais tarehe 3 Mei, 2016 na waliweza kushiriki. Tukio la mwisho ambalo Mzee wetu Mrema alishiriki ni katika Kongamano la Kitaifa la miaka 58 ya Muungano lililofanyika Dodoma tarehe 26 Aprili, 2022 ambalo liliambatana na uzinduzi wa Kitabu cha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: Chimbuko, Misingi na Maendeleo, katika tukio hili wenzake watatu hawakuweza kushiriki kutokana na changamoto za kiafya.

Hakika Mzee Hasanieli Mrema atabaki katika kumbukumbu zetu daima.

**Ndugu Waombolezaji:**

Ofisi ya Makamu wa Rais licha ya kushiriki katika kuhudumia msiba huu, inatoa Rambirambi ya shilingi **5,000,000.00**. Tutaendelea kuwaombea ili Mwenyezi Mungu awape nguvu na ustahimilivu katika kipindi hiki kigumu.